UHURU UK 15.

kila mwaka nchini

# Sekta ya uvuvi Kigoma yapewa boti ya ulinzi

Na MWANDISHI WETU, Kigoma

KAMPUNI inayotoa huduma za usambazaji kimataifa ya DHL Express, imetoa msaada wa boti ya ulinzi kwa wavuvi wa mkoani Kigoma.

Akizungumza wakati wa makabidhiano ya boti hiyo, mwishoni mwa wiki, Mkurugenzi Mtendaji wa DHL Express Tanzania, Paul Makolosi, alisema msaada huo katika sekta ya uvuvi mkoani hapa utasaidia wavuvi kufanya kazi zao kwa ufanisi eneo la Ziwa Tanganyika.

Pia, alisema itawasaidia wavuvi kuvua samaki kwa usalama zaidi na kufikia malengo waliyojiwekea.

"DHL imekuwa ikifanya mambo mbalimbali ya kusaidia maisha ya wengi. Kampuni tunafanya kile ambacho kipo ndani ya uwezo wetu, siyo tu kampuni ya kusambaza vifurushi, lakini tumekuwa tukisaidia mambo mbalimbali kwa jamii inayotuzunguka," alisema.

Aliongeza kuwa wamekuwa wakiwaunga mkono wakazi wa mkoa huo wakiwemo wavuvi kwa kufanya nao kazi kwa ufanisi kuhakikisha wanafikia malengo yao kwa usalama zaidi na kusafirisha bidhaa sehemu mbalimbali.

"Tumepiga hatua kubwa katika kuwezesha upatikanaji wa vifaa kwa kupanua wigo wetu kote nchini na kuongeza utaalamu wetu wa kimataifa, kuhakikisha tunaweza kutoa huduma za haraka za kiwango cha kimataifa kwa wateja wetu na kuunganisha Tanzania na dunia kwa ujumla," aliongeza.

Kwa upande wake, Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, alishukuru DHL kutokana na msaada huo na kusema anaamini wavuvi watafanya kazi zao kwa usalama zaidi.

> "DHL imekuwa ikifanya mambo mbalimbali ya kusaidia maisha ya wengi. Kampuni tunafanya kile ambacho kipo ndani ya uwezo wetu, siyo tu kampuni ya kusambaza vifurushi, lakini tumekuwa tukisaidia...
>
> Mkurugenzi Mtendaji wa DHL Express Tanzania, Paul Makolosi.

"Ninaishukuru DHL Express Tanzania, kutokana na kazi nzuri wanazoendelea kuzifanya kwa jamii, kuhakikisha kampuni yao inaendelea kupata mafanikio na kufikia malengo waliyojiwekea."

"Wameamua kutoa mchango wa boti ya ulinzi kwa wavuvi wa Kigoma, unamaanisha kwamba DHL imekuwa karibu ya jamii kwa kiasi kikubwa na kuendelea kutoa sapoti katika sekta ya uvuvi Tanzania," alisema.

Aliongeza kuwa: "Tunatambua sekta ya uvuvi imebadilika na kuwa shughuli muhimu ya kiuchumi, badala ya kuwa suala la mazingira au viumbe hai, hivyo ni lazima tulinde na kulinda maji yetu."

Ofisa Mtendaji Mkuu wa DHL kwa nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara, Fatima Sullivan alisema: "Kwa kichocheo cha biashara na uwekezaji wenye athari nyingi kwa uchumi mpana wa kijamii na kiuchumi, DHL imeendelea kunufaisha biashara zinazojenga mauzo ya nje nchini na huduma kwa wakati."

Aliendelea kusema kuwa: "Taarifa za utoaji, ukiangalia zaidi ya mtazamo wa biashara, uwajibikaji wa kampuni ni sehemu muhimu ya mkakati wetu wa ushirika na Kigoma ni jiji ambalo liko karibu na mioyo yetu nchini. Tunafurahi tunaweza kutumia rasilimali zetu ili kusaidia jamii kwa njia chanya."

MWANANCHI 4K20

## Kwa Ufupi

# Waziri alia mchango mdogo wa mifugo

**Morogoro**. Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki amesemali cha ya Tanzania kuongoza kwa idadi ya mifugo barani Afrika, bado mchango wa mifugo kiuchumi ni mdogo.

Alisema hayo jana kwenye mkutano wa 12 wa wadau wa malisho ulioandaliwa na Chama cha Nyanda za Malisho Tanzania (RST).

"Kuna mifugo ilikufa mwaka jana na mwanzoni mwa mwaka huu kwa sababu hatukutaka kuingia gkuanatajirika bure, lazima tubadilike," alisema.

Alisema wizara inaandaa mwongozo wa malisho utakaosaidia kuweka mwelekeo kwa mfugaji.

Mwenyetiki wa RST, Said Seleman alisema nyanda za malisho zinaharibiwa kila siku kutokana na matumizi yasiyo endelevu.

**(Lilian Lucas)**

Scanned with CamScanner